

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE

05 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 05 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

370. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ulianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya Mwaka 2010 na lengo la Mfuko huo ni kusaidia Baraza la Watu Wenye Ulemavu kufanya kazi zake kwa ufanisi, kuendesha tafiti mbalimbali na kubaini changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu, lakini Mfuko huo haukutengewa fedha katika Bajeti ya mwaka 2016/2017:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya Mfuko huo ili uweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

371. MHESHIMIWA ESTER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Wilaya ya Siha kimeonekana kukidhi mahitaji yote muhimu tayari kwa usajili lakini hadi sasa Kituo hicho hakijapata usajili wa Hospitali ya Wilaya:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kupandisha hadhi Kituo hicho ili kupunguza kadhia ya upatikanaji wa huduma za kiafya kwa Wananchi wa Wilaya ya Siha.

372. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je Serikali haioni haja sasa ya kuziagiza rasmi Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza baadhi ya majukumu yake ili Walimu wapate huduma stahiki kwa wakati.

373. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunga mkono Wananchi wa Kata ya Haneti kwa kumaliza ujenzi wa chumba cha upasuaji ambacho kilianzishwa kwa nguvu za Wananchi na Mfuko wa Jimbo.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

374. MHESHIMIWA JOHN WEGESA HECHE (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wilaya ya Tarime ni miongoni mwa Wilaya zinazoongoza kwa wakazi wake kuwa na kesi za kubambikiwa hasa za wizi wa kutumia silaha na mauaji, kitendo kinachokuwa na sura ya kumpa mtuhumiwa wakati mgumu sana kupata msaada wa Kisheria:-

Je, ni kwa nini Serikali isisaidie upatikanaji wa msaada wa Kisheria kwa mahabusu hao ambao kitakwimu ni wengi katika Gereza la Tarime kuliko mashauri mengine yeyote.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**375. MHESHIMIWA ZUBEDA HASSAN SAKURU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na
vifo vya Watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

**376. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-
Wastani wa juu wa kuzaa kwa Mwanamke wa
Kigoma ni mara saba juu ya wastani wa Kitaifa
lakini Wanawake hawa wana hatari ya kupoteza
maisha wakiwa wanajifungua kutokana na
miundombinu mibovu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha
uzazi salama na kutokomeza kabisa vifo vya
Mama na Mtoto.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

377. MHESHIMIWA DKT. HADJI HUSSEIN MPONDA (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali kupitia aliyekuwa Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda ilitoa agizo la kuweka utatuzi wa kudumu katika migogoro ya ardhi iliyopo baina ya Wananchi na Serikali katika maeneo ya Vijiji na Mapori Tengefu. Aidha, katika kampeni zake Wilayani Malinyi Mheshimiwa Rais aliahidi uhaulishwaji wa 'Buffer Zone' ya Pori Tengefu la Kilombero kwa Vijiji vinavyopakana ili wawe huru katika shughuli zao lakini hadi leo hakuna utekelezaji wowote:-

- (a) Je, utekelezaji wa ahadi na agizo hili umefikia wapi;
- (b) Je, Serikali ina mpango mbadala kwa Wananchi wanaoishi kihalali katika maeneo hayo ya 'Buffer Zone' ya Pori Tengefu la Kilombero.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

378. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya suala la kilimo cha umwagiliaji katika Kijiji cha Chomache, Nkote hasa ikizingatiwa kuwa wataalam wa kilimo walikuja kufanya utafiti na kueleza mpango wa kuchimba Bwawa kwa ajili hiyo pale Choma.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

379. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- (a) Je, Ranchi ya Missenyi ina Ng'ombe wangapi kwa sasa;
- (b) Je, Wananchi wanaoizunguka Ranchi hiyo wananufaikaje kutokana na uwepo wake.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
05 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**